JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA WAZIRI MKUU

# SERA, BUNGE, URATIBU NA WENYE ULEMAVU



KATIBU MKUU
OFISI YA WAZIRI MKUU
2 BARABARA YA POSTA
40412 DODOMA

JARIDA LA MTANDAONI • WWW.OWM.GO.TZ • JANUARI 2026



# WENYE ULEMAVU WA NGOZI KUNUFAIKA NA MFUKO WA ULEMAVU NCHINI – NAIBU WAZIRI NDERIANANGA

Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge Uratibu na Wenye Ulemavu Mhe. Ummy Nderiananga, amesema Watu wenye Ulemavu wa Ngozi wapo Mbioni kunufaika na Mfuko wa Wenye Ulemavu wa Ngozi kwa kupata mafuta maalum kwa matumizi ya ngozi.

Ameyasema hayo Bungeni Jijini Dodoma katika Bunge la 13 Mkutani wa Pili Kikao cha Nne, wakati akijibu swali la nyongeza lililoulizwa na Mhe. Stella Ikupa Alex (Mb) Viti Maalum CCM lililohoji ni Lini Serikali itatoa mafuta ya watu wenye ulemavu wa ngozi katika Halmashauri nchini.

Mhe. Nderiananga amesema kuwa, Serikali inatambua uhitaji wa mafuta kwa watu wenye ulemavu wa ngozi nchini na kufafanua kwamba kwa kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, kupitia mfuko wa wenye Ulemavu nchini serikali imetenga fedha maalum na kuzielekeza Kilimanjaro Catholic Medical Centre (KCMC) ili kuweza kuzalisha mafuta mengi zaidi na kuyasambaza.

Aliongeza kuwa, kupitia Wizara ya Elimu, Serikali inasambaza mafuta hayo ili kuweza kuwafikia wanafunzi wenye ulemavu wa ngozi na yananunuliwa kama vifaa saidizi.

"*Tuna hospitali teule kama vile Bugando yanafanyika matibabu hayo ya kufanya uchunguzi wa ngozi kwa ajili ya kutambua aina ya ngozi kwa watoto ili kuwapatia matibabu sahihi na Serikali ina lengo la kusambaza huduma hizo mpaka vijijini*" amefafanua.



# IFAD YAAHIDI KUENDELEZA SEKTA YA KILIMO NA UVUVI TANZANIA

Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo (IFAD) umehakikishia Serikali ya Tanzania kuendelea kuimarisha ushirikiano wa kimkakati katika kukuza sekta za Kilimo na Uvuvi, hususan kwa kuwainua wakulima na wavuvi wa vijijini.

Akizungumza, Katibu Mkuu wa Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu), Dkt. Jim Yonazi, amekutana na Mkurugenzi Mkazi wa IFAD, Bw. Sakphouseth Meng, ambapo IFAD imethibitisha kuendelea kutoa mikopo na rasilimali fedha kwa miradi ya maendeleo.






# WATANZANIA WAHIMIZWA KUCHANGAMKIA FURSA UJENZI WA UWANJA MPYA WA AFCON ARUSHA

Watanzania wameaswa kuchangamkia fursa mbalimbali za kiuchumi zinazotokana na ujenzi wa uwanja mpya wa mpira wa miguu unaoendelea kujengwa Jijini Arusha kwa ajili ya michuano ya Mataifa ya Afrika (AFCON) mwaka 2027.

Wito huo umetolewa na Mwenyekiti wa Kamati ya Makatibu Wakuu, ambaye pia ni Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu), Dkt. Jim Yonazi, wakati wa ziara ya kamati hiyo ya kukagua maendeleo ya mradi huo unaoendelea Jijini Arusha.

Akizungumza baada ya ziara hiyo, Dkt. Yonazi ameeleza kuridhishwa na kasi ya ujenzi huo ambao kwa sasa umefikia asilimia 74, huku akisisitiza kuwa uwanja huo ni uwekezaji wa kimkakati utakaoleta tija kwa taifa hata baada ya kumalizika kwa mashindano hayo.

"Ujenzi huu umefikia hatua nzuri na utakamilika kwa wakati, niwaombe Watanzania wachangamkie fursa zinazojitokeza sasa wakati wa ujenzi na hata baada ya kukamilika kwani uwanja huu utaendelea kutumika kwa mashindano ya ndani na kimataifa," amesema Dkt. Yonazi.

Aidha, Dkt. Yonazi amebainisha kuwa, usimamizi wa mradi huo unazingatia viwango vya juu vya ubora, ikiwemo kuweka miundombinu rafiki kwa watu wenye mahitaji maalum, ili kuhakikisha huduma zote zinapatikana kwa usawa kwa wageni na wenyeji watakaotembelea eneo hilo.

Uwanja wa Arusha ni miongoni mwa miundombinu muhimu inayotayarishwa na Serikali ya Tanzania, ambayo ni mshiriki mwenza katika uenyeji wa michuano ya AFCON 2027, ikishirikiana na nchi za Kenya na Uganda.

Kukamilika kwa uwanja huo kunatarajiwa kuchochea ukuaji wa sekta ya utalii wa michezo jijini Arusha, kutokana na nafasi ya jiji hilo kama kitovu cha utalii katika Ukanda wa Afrika Mashariki.







# SERIKALI KUSHIRIKIANA NA VYUO VIKUU KUIMARISHA UWAJIBIKAJI KATIKA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA UMMA

Ofisi ya Waziri Mkuu (SBUU) imesaini Hati za Mashirikiano (MoU) na Vyuo Vikuu vinne ambavyo ni Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), Chuo Kikuu Mzumbe (MU), Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM) na Taasisi ya Uhasibu (TIA) kwa lengo la kuimarisha mfumo wa ufuatiliaji na tathmini unaotumia ushahidi katika utekelezaji wa sera, mipango na miradi ya maendeleo.

Katibu Mkuu Dkt. Jim Yonazi amesema, ushirikiano huo utaongeza uwezo wa wataalamu wa ufuatiliaji na tathmini, kukuza tafiti bunifu na kuhakikisha maarifa ya vyuoni yanaboresha utendaji wa Serikali.

Aidha, Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dodoma, Prof. Lughano Kusiluka, amesema Vyuo Vikuu vina dhamira ya kushirikiana na Serikali katika kuimarisha Ufuatiliaji na Tathmini kama nyenzo muhimu ya maendeleo ya taifa, ili Tanzania iwe mfano wa kuigwa na nchi nyingine katika matumizi ya ushahidi kwenye maamuzi ya maendeleo.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Idara ya Ufuatiliaji na Tathmini ya Utendaji wa Serikali, Bi. Sakina Mwinyimkuu, amesema ushirikiano huo una lengo la kujenga tamaduni ya uwajibikaji, kuimarisha utendaji wa taasisi za umma na kuongeza mchango wa kitaalamu katika kufanikisha maendeleo yenye tija kwa wananchi.







# OFISI YA WAZIRI MKUU YAKABIDHI VIFAA VYA MISAADA YA KIBINADAMU KWA WAATHIRIKA WA MAFURIKO KILOSA

Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu) kupitia Idara ya Menejimenti ya Maafa  imekabidhi vifaa mbalimbali vya misaada ya kibinadamu kwa Mkuu wa Wilaya ya Kilosa kwa Ajili ya waathirika wa Mafuriko Katika Kata ya Tindiga Wilaya ya Kilosa Mkoani Morogoro.

Makabidhiano ya vifaa hivyo yamefanyika Katika Ofisi ya Mkuu wa Wilaya na yameongozwa na Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu Dkt. James Kilabuko, Mkurugenzi wa Idara ya Menejimenti ya Maafa Brig. Jen. Hosea Ndagala na kapokelewa na Mkuu wa Wilaya ya Kilosa Mheshimiwa Shaka Hamdu Shaka akiwa na kamati ya ulinzi na usalama ya Wilaya.

Vifaa hivyo vilivyokabidhiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu kupitia Idara ya Menejimenti ya Maafa ni Magodoro 90, Vyandarua 90, Mablanketi 90, Mahema 5 pamoja na Ndoo 90. Pia Ofisi ya Waziri Mkuu imetoa Unga Tani 7.2, Maharage Tani 2.1, Mafuta ya Kupikia Lita 360, Chumvi Kilo 300 na Sukari Kilo 600.








# UANDAAJI UTEKELEZAJI WA MIONGOZO YA UFUATILIAJI NA TATHMINI SERIKALINI KUONGEZA KASI YA UKAMILISHAJI WA MIRADI YA MENDELEO NCHINI

Zoezi la uandaaji na utekelezaji wa Miongozo ya Ufuatiliaji na Tathmini Serikalini limeelezwa kuwa chachu muhimu ya kuongeza kasi ya ukamilishaji wa miradi ya maendeleo nchini.

Akizungumza kwa niaba ya Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu, Dkt. Jim Yonazi, Naibu Katibu Mkuu Dkt. James Henry Kilabuko amesema miongozo hiyo inarahisisha utekelezaji wa miradi na kuhakikisha matokeo chanya yanawafikia wananchi kwa wakati.

Aidha, amesisitiza matumizi ya Muongozo Jumuishi wa Ufuatiliaji na Tathmini (Juni 2024) unaotumia dhana ya Whole of Government Approach ili kuimarisha uwajibikaji na utendaji Serikalini.

Wakurugenzi wa Halmashauri wametakiwa kuzipa rasilimali za kutosha Vitengo vya Ufuatiliaji na Tathmini vilivyoanzishwa Aprili 2024, huku Maafisa Mipango wakihimizwa kuzingatia viashiria vya U&T tangu hatua za awali za mipango.

Kikao kazi hicho kimefanyika Mkoa wa Iringa kikihusisha Wakurugenzi, Maafisa Mipango na Wakuu wa Vitengo vya Ufuatiliaji na Tathmini kutoka Mamlaka za Serikali za Mitaa.







# DKT. KILABUKO AZINDUA NYARAKA ZA USIMAMIZI WA MAAFA NKASI

Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu), Dkt. James Kilabuko amezindua Nyaraka za Usimamizi wa Maafa katika Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi, mkoani Rukwa.

Akizungumza wakati wa uzinduzi huo, Dkt. Kilabuko amesisitiza nyaraka hizo kutekelezwa kwa vitendo, akibainisha kuwa ni msingi muhimu wa kujiandaa na kukabiliana na majanga yanapojitokeza.

Ameeleza kuwa utekelezaji wa nyaraka hizo utaimarisha:

- Ushirikishwaji wa jamii na wadau
- Mfumo wa tahadhari za mapema
- Uwezo wa kuzuia, kupunguza madhara na kurejesha hali baada ya maafa.

Dkt. Kilabuko amesema Wilaya ya Nkasi imekuwa ikikabiliwa na majanga mbalimbali ikiwemo upepo mkali, mafuriko, magonjwa ya mlipuko, mgongano wa binadamu na wanyamapori, pamoja na majanga mengine kama ajali, moto na maporomoko ya ardhi.

Aidha, amezipongeza mamlaka za Wilaya kwa jitihada za kudhibiti mlipuko wa ugonjwa wa kipindupindu, na kuishukuru UNICEF kwa ufadhili uliowezesha uandaaji wa Mpango wa Kukabiliana na Maafa na Mkakati wa Kupunguza Vihatarishi vya Maafa.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU**




Pakua jarida hili kupitia:
www.pmo.go.tz

## Jarida hili hutolewa na:

Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge, Uratibu
na Wenye Ulemavu